



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA**



SEPTEMBER 28, 2021

**MWONGOZO WA KUJISAJILI KAMA MTEJA (CLIENT) KWENYE MFUMO
JUMUISHI WA MNRT (MNRT PORTAL)**

Mfumo Jumuishi wa MNRT (MNRT Portal), ni mfumo ambayo unahuduma mbalimbali kama **kusajili watafiti, kutoa vibali vya kufanya utafiti, kuchapisha maandiko ya utafiti, kanzidata ya tafiti za misitu na ufugaji nyuki**, na n.k., kwaajili ya Wadau wa Misitu, Nyuki, Utalii, Uwindaji na Makumbusho. Lakini mteja (client) anatakiwa kuunganishwa na mfumo huu ili aweze kutumia huduma zipatikanazo na mfumo.

Mteja anajisajili vipi kwenye Mfumo Jumuishi wa MNRT (MNRT Portal)?

Mteja anatakiwa kufika Wizara ya Maliasili na Utalii au anaweza kwenda kwenye kituo chochote cha taasisi zifuatazo akiwa na kitambulisho cha NIDA au leseni ya udereva ya kuendeshea magari:

1. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI);
2. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS);
3. Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA);
4. Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRD);
5. Makumbusho ya Taifa;
6. Chuo cha Utalii; na
7. Malikale

Imetolewa na,

Kitengo cha Usajili Watafiti, Miradi na Kamati ya Maadili ya Utafiti